



Neema aliwaza sana kuhusu siku yake ya kuzaliwa. Alimuuliza rafiki yake, "Je siku yako ya kuzaliwa ni kama yangu? Mama aliniambia kuwa nilizaliwa tarehe 29 mwezi Februari."




Akiwa nyumbani Neema alimuuliza Mama yake, "Mama! Mwaka jana siku yangu ya kuzaliwa haikufika. Mbona rafiki yangu Ana anafanya sherehe yake kila mwaka?"



Mama akasema, "Subiri tu mwanangu siku yako ya kuzaliwa itafika tu. Siku ikifika tutafanya sherehe kubwa. Pia tutawaalika rafiki zako."



Neema akamjibu Mama yake na kusema,
“Lakini Mama mwaka jana nilisubiri sana.
Mwaka uliisha siku hiyo haikufika.”




Akaendelea kusema, "Rafiki yangu Ana tulimpa hongera, tulikula na kuimba. Sote tukafurahi sana. Napenda pia niwaalike marafiki tule, tucheze na kuimba."



Mama akamjibu, "Basi mwanangu usihuzunike sana wiki ijayo tutafanya sherehe ya siku ya kuzaliwa kwako. Neema aliingia ndani kwa huzuni. Alijua Mama hamwambii ukweli.



Baada ya wiki moja kupita, siku ya kuzaliwa Neema ilifika. Neema alifurahi sana kuona anaandaliwa sherehe. Akasema, "Nimefurahi sana, leo ni siku yangu ya kuzaliwa."



Marafiki wa Neema walifika na zawadi nyingi. Baba na Mama pia, walimpa zawadi. Walimvisha kofia nzuri yenyе rangi za kupendeza. Neema alichukua zawadi zake na kuzitazama.

Zawadi zilikuwa nyingi na nzuri mno. Mama akamwambia, "Neema siku hii huja mwaka mkuu, yaani mara moja kila baada ya miaka minne."